JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

# TAARIFA KWA UMMA

## MIFUMO YA TIKETI MTANDAO ISIYOIDHINISHWA MWISHO JUNI 30, 2025

***Mwanza, Juni 23, 2025***

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inaendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Tiketi Mtandao za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024 zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 20 la tarehe 12 Januari 2024. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, watoa huduma za mifumo ya tiketi mtandao wanapaswa kuwa wameidhinishwa na LATRA.

Katika utekelezaji wa kanuni hizo, Mamlaka inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), watoa huduma za mifumo ya tiketi mtandao, wamiliki wa mabasi na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) ili kurahisisha utoaji wa huduma za usafiri.

Mamlaka inawakumbusha watoa huduma za mifumo ya tiketi mtandao kukamilisha matakwa ya usajili kwa mujibu wa Sheria kabla ya tarehe 1 Julai 2025. Mifumo hiyo itapewa kibali baada ya Mamlaka kujiridhisha kuwa imekidhi vigezo, ikiwa ni pamoja na kuwa imeunganishwa na mfumo wa TRA wa EFDMS na Mfumo Mama wa Tiketi Mtandao (CeTS). Ifikapo tarehe hiyo, watoa huduma ya mifumo ya tiketi mtandao ambao hawajaidhinishwa hawataruhusiwa kutoa huduma.

Mamlaka inatoa rai kwa wasafirishaji kuhakikisha kuwa wanahudumiwa na watoa huduma za mifumo walioidhinishwa ili kujiepusha na adha inayoweza kujitokeza.

Digitally Signed By Salum PAZZY
Mon Jun 23 22:08:36 EAT 2025

Salum PAZZY

**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**

LATRA Makao Makuu, S. L. P. 1742, 41104 Tambukareli, Dodoma
Simu + 255 262 323 930, Barua pepe: dg@latra.go.tz , info@latra.go.tz , Tovuti: www.latra.go.tz